

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA



27/4/2022.

TANGAZO

TANGAZO LA ZABUNI YA UWAKALA WA UKUSANYAJI WA USHURU WA MAPATO HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA

Halmashauri ya Wilaya ya Muheza inawatangazia wafanyabiashara/makampuni/ushirika/vikundi kuwa inahitaji kupata wazabuni wenye uwezo wa kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Zabuni zinazotangazwa ni kama ifuatavyo ;

ZABUNI NAMBA	JINA LA ZABUNI
LGA/132/2021/2022/NC/25	Uwakala Wa Kukusanya Ushuru Wa mchanga

3. Masharti kwa Waombaji:-

1. Mwombaji awe na uwezo wa kukusanya mapato kwa kutumia mfumo wa Kielekroniki (Electronic Revenue Collection System).
 - i. Mfumo wa kielekroniki unaotumika na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ni Local Government Revenue Collection Information System – LGRCIS.
 - ii. Wakala atatakiwa kuonyesha idadi ya **(Point of Sale- POS Machine)** atakazotumia, ikiwa ni pamoja na maeneo zitakapotumika (vituo vya kukusanya mapato). Muombaji atakayefanikiwa kupata kazi atatakiwa kutumia mashine za kukusanya mapato ambazo zimeunganishwa na mfumo wa mapato wa Halmashauri
 - iii. Stakabadhi zitakazotumika kukusanya ushuru zitapatikana Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na zitakuwa ni za mfumo wa kietroniki
 - iv. Mapato yote yatakayokusanywa na wakala yataingizwa katika Akaunti ya Halmashauri na wakala atalipwa kwa asilimia. Muda wa malipo kwa wakala ni ndani ya siku saba [7] ya mwezi unaofuata baada ya wakala kuleta hati ya madai husika.
 - v. Kila mwombaji anatakiwa kufanya utafiti kwenye eneo la mapato analotarajia kuomba na kuonyesha kiasi cha mapato atakachokusanya kwa kila mwezi.
 - vi. Wakala atawajibika kuwasilisha makusanyo katika akaunti ya Halmashauri kila jumanne na Ijumaa kila wiki (**mawasilisho yatafanyika mara mbili kwa wiki**)
- vii. Wakala aonyeshe asilimia itakayolipwa baina yake na Halmashauri pamoja na mchanganuo wa mapato, matumizi na faida. Na ikumbukwe kwamba kuweka kiwango kidogo cha asilimia ya malipo sio kigezo pekee cha kupata zabuni,

mchangunuo wa mapato na matumizi ndio utakao toa picha ya uhalisia wa kiwango cha asilimia

- viii. Gharama za ukusanyaji ushuru ni juu ya wakala mwenyewe
- ix. Muombaji awe na Leseni hai na inayofanana na Biashara husika
- x. Usajili wa TIN/VAT
- xi. Uthibitisho wa ulipaji kodi (Tax clearance certificate)
- xii. Muombaji awe na usajili wa kuandikishwa kwa Kampuni.
- xiii. Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (Power of attorney) wa mtu atayehusika na zabuni hii
- xiv. Muombaji awe na uzoefu katika ukusanyaji wa mapato siopungua mwaka mmoja. (Ambatanishe na barua za uteuzi wa kazi hizo).
- xv. Muombaji ataje eneo la Kampuni au biashara ilipo (physical location)
- xvi. Viwango vya kutoza ushuru ni vile vinavyopitishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kulingana na sheria ndogo
- xvii. Muombaji awasilishe mpango kazi wa kuonyesha jinsi atavyotekeleza kazi hiyo.
- xviii. Asilimia 20% ya ujira wake ya kiwango anachotakiwa kulipwa Wakala kitatozwa kwa wakala atakaye chelewesha marejesho yake ndani ya siku 5 kulingana na tarehe ya marejesho ya mkataba.
- xix. Muombaji aonyeshe uwezo wa kifedha wa kufanya kazi. Aambatanishe Bank statement ya kuanzia mwezi January 2022 hadi Marchi 2022.
- xx. Muombaji hatakiwi kuwa mtumishi au Kiongozi wa Halmashauri ya wilaya muheza.
- xxi. Zabuni zote zitapokelewa kwenye mfumo wa **Taneps**
- xxii. Aonyeshe idadi ya POS atakazotumia na mahali(vituo/ollection point)
- xxiii. Muombaji asiwe na mgogoro na Halmshauri

JINSI YA KURUDISHA ZABUNI

Muombaji atatakiwa kujaza fomu husika na kutoa maelezo kwa ufasaha kulingana na maelezo yaliyopo katika kabrasha la Zabuni.

Kabrasha la Zabuni baada ya kujaza kama ilivyoelezwa litumwe kwenye mfumo wa Taneps.

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P. 20,
Muheza.**